




# Kanuni za KBR za Maadili ya Biashara



## Sisi Ni Watu Waadilifu



# Orodha ya Yaliyomo


**Ujumbe kutoka kwa Stuart Bradie, Rais na Afisa Mkuu Mtendaji** 2

**Sisi Ni Watu Waadilifu** 3
- Maono na Maadili Yetu 4
- Kanuni Zetu za Maadili 5
- Wajibu Wetu 6
- Jinsi Tunavyofanya Maamuzi 7
- Jinsi Tunavyoomba Msaada, Kuripoti na Kuuliza Maswali 8
- Tunaheshimu Usiri na Kuficha Utambulisho 9
- Hatukubali Kulipiza Kisasi 9

**Kuthamini Kila Mmoja Wetu** 10
- Tunadumisha Afya na Usalama wa Wafanyakazi na Makontrata Wetu 11
- Tunahimiza Mazingira ya Heshima Kazini 12

**Kutoa Huduma kwa Uadilifu** 14
- Tunazuia Ukinzani wa Maslahi 15
- Tunazuia Hongo na Ufisadi 17
- Tunatoa na Kupokea Zawadi za Kibiashara kwa Uwajibikaji 19
- Tunaendesha Kazi na Biashara ya Kimataifa kwa Uadilifu 20
- Tunashindana kwa Njia ya Haki 21
- Tunatenda kwa Ukweli 22

**Kuthamini Raslimali Zetu Muhimu** 23
- Tunalinda Faragha na Maelezo ya Binafsi 24
- Tunalinda Sifa Yetu 25
- Tunalinda Maelezo ya Siri na ya Kampuni 26
- Tunazuia Biashara ya Kindani 27

**Kutoa Huduma kwa Uwazi** 28
- Tunafanya Kazi kwa Uadilifu na Uwazi na Wateja wa Serikali 29
- Tunafanya Kazi kwa Uadilifu na Wauzaji na Washirika Wengine 30
- Tunaweka Rekodi na Akaunti Sahihi 31

**Kuthamini Jamii Zetu** 32
- Tunajenga Mustakabali wa Kudumu 33
- Tunaheshimu Haki za Binadamu 34
- Tunashirikiana na Jamii Zetu 35

**Nyenzo na Kuripoti** 36



Stuart Bradie
Rais na Afisa Mkuu Mtendaji

# Ujumbe kutoka kwa Stuart Bradie, Rais na Afisa Mkuu Mtendaji

Katika KBR, tumejenga sifa kuu kwa kutoa suluhu kwa wateja wetu, na wafanyakazi wetu wamejitahidi kila wakati kuwa bora katika kazi zao. Kufanya kazi kwa ubora kunamaanisha kutoa huduma kwa uadilifu. Uadilifu unahitaji ukweli, na ukweli unaleta uaminifu.

Kanuni Zetu za Maadili ya Biashara ("Kanuni") ni muhimu kulingana na jinsi sisi kama timu tunavyoshirikiana na mazingira yetu na kuleta mafanikio pia. Kanuni hizi zinalingana na Maadili ya KBR MOJA (ONE KBR Values), na, kimahususi, kanuni ya "Sisi ni Watu Waadilifu" inayotuongoza katika kila kitu tunachofanya.

Kanuni za KBR zimeboreshwa ili kuwapa wafanyakazi wote mwongozo amilifu katika shughuli za kila siku. Kanuni zetu zinatoa mwongozo maalum ambao unahusu kila mmoja wetu, bila kujali biashara, eneo au idara. Ni muhimu tuufuate ili kuimarisha zaidi utamaduni wetu wa uadilifu na kulinda usalama wetu na wa kampuni.

Hata hivyo, Kanuni hizi zinaweza kukosa kuangazia kila hali, na ndiyo sababu lazima tuongozwe na maadili yetu, hasa, uadilifu. Nimejitolea kwa moyo wote kukuza utamaduni ambapo wafanyakazi wanahisi kuwa na uwezo wa kuripoti masuala yoyote kuhusu uwezekano wa kutekeleza mwenendo au tabia mbaya ambazo ni kinyume na Kanuni na maadili yetu bila uoga wowote wa kulipiza kisasi, ili matatizo yoyote yaweze kushughulikiwa haraka iwezekanavyo.

Huenda kukawa na hali ambapo una swali kuhusu masuala fulani ya utiifu au uadilifu yanayokuhusu. Tafadhali omba ushauri au ufafanuzi kutoka kwa meneja wako au kwa nyenzo zilizoorodheshwa katika Kanuni zetu. Huduma ya Dharura ya Maadili ya KBR (KBR Ethics Hotline) ni moja ya nyenzo hizo ambayo inakuwezesha kuwasiliana na Timu ya Uadilifu katika Biashara (Business Integrity Team) kwa siri au bila kujitambulisha.

Ninajivunia KBR, maadili yake na kwamba Sisi ni Watu Waadilifu kila siku. Na nina matumaini kwamba sisi sote tutaendelea kufanya kazi pamoja tukidumisha viwango vya juu zaidi vya uadilifu ili tuweze kutimiza ahadi zetu kwa usalama na kwa uendelevu na kusaidia kila mmoja wetu na wateja wetu sasa na siku za usoni.




# Sisi Ni Watu Waadilifu

- Maono na Maadili Yetu
- Kanuni Zetu za Maadili
- Wajibu Wetu
- Jinsi Tunavyofanya Maamuzi
- Jinsi Tunavyoomba Msaada, Kuripoti na Kuuliza Maswali
- Tunaheshimu Usiri na Kuficha Utambulisho
- Hatukubali Kulipiza Kisasi

# Maono na Maadili Yetu

Tunajitahidi kuunda ulimwengu bora, salama zaidi na wa kudumu kwa kuwaleta pamoja wafanyakazi bora na mahiri zaidi ili kutoa huduma ya teknolojia na suluhu ambazo zinawasaidia wateja wetu kutimiza dhamira na malengo yao muhimu zaidi.

Maadili yetu ni kanuni zetu muhimu na za kudumu ambazo zinaendesha shughuli zetu za kila siku za biashara na kutubainisha sisi kama kampuni.




## Tunathamini Wafanyakazi Wetu

Wafanyakazi wetu ni kiini cha kila kitu tunachofanya. Tumejitolea kuunda mazingira anuwai na jumuishi ya kazi ambapo kila mfanyakazi wetu anahisi kuwa salama, kusaidika, kuheshimika, kuaminika na kuthaminiwa, na ambapo kila mtu anapewa fursa za kukua na kufikia uwezo wake kamili.

## Tunatimiza Ahadi Zetu

Sisi ni washirika wa kuaminiwa na wateja wetu. Hatubadilishi msimamo wetu wa kujitolea kuunda suluhu bunifu za kiteknolojia za ubora wa juu kwa ajili yao, na thamani ya kipekee ya kudumu kwa wadau wetu wote, zilizojengwa kwa msingi thabiti wa kibiashara na nidhamu ya utendakazi.

## Sisi Ni Watu Waadilifu

Sisi ni watu waadilifu, tunaothamini ukweli, uaminifu, ujasiri, haki, busara na ukakamavu. Tunaamini kwamba kutendea haki ulimwengu, jamii za mahali ambapo tunaishi na kufanya kazi na wafanyakazi wetu kuna manufaa kwa biashara yetu. Hatulegezi msimamo wetu wa uadilifu.

## Tunawezesha

Tunawezesha wafanyakazi wetu wote kupitia lengo la pamoja, zana sahihi na utamaduni wenye msaada wanaohitaji ili kuchukua hatua mapema, kukubali mabadiliko na kufaulu. Tunawaamini kuwa waamuzi wa kujitegemea ambao hawaogopi kukabiliana na changamoto yoyote ana kwa ana na wanaojivunia kumiliki kazi yao.

## Sisi Ni Timu ya Jumla

Tuna nia ya kufaulu, kibinafsi na kama kampuni, lakini tunathamini mafanikio ya timu yetu ya jumla kuliko mafanikio yetu ya kibinafsi. Lengo letu la pamoja linaendesha ubora wa utendakazi wetu, linachochea ari yetu ya kutimiza mahitaji ya wateja wetu, na kutufanya kuwa kampuni bora, thabiti, inayofaa zaidi na yenye utendaji bora. Sisi ni KBR MOJA.

# Kanuni Zetu za Maadili

Kanuni zetu za Maadili ya Biashara zinabainisha kikundi cha viwango vya uadilifu na kanuni za kisheria kwa kila mtu anayefanyia kazi au anayefanya kazi kwa niaba ya KBR. Tunafanya biashara yetu kwa kutii Kanuni zetu na sheria zote husika. Tunatarajia pia washirika wetu wa biashara wanaofanya kazi na, au kwa niaba ya KBR kufuata viwango hivi vya uadilifu.

Kanuni hizi zinatumika kama mwongozo wa jinsi tunavyofanya biashara na kushirikiana na wateja wetu, jamii zetu na kila mmoja wetu.

## Ikiwa hatufanyi kwa uadilifu, hatufanyi ipasavyo!

Ukiukaji wowote wa Kanuni hizi au sheria unaweza kusababisha kuchukuliwa hatua ya kinidhamu, ikiwa ni pamoja na hata kufutwa kazi. Soma, elewa na utii Kanuni zetu. Shiriki katika mafunzo yoyote yanayohusiana na Kanuni zetu, na ujue jinsi zinavyotumika kwenye wajibu wako katika KBR. Kama KBR MOJA, uadilifu wetu unategemea kutii Kanuni zetu.





# Wajibu Wetu

**Sote tuna wajibu wa kutenda mambo kulingana na Kanuni zetu. Kama wafanyakazi:**

- Tunatenda kwa ukweli na uadilifu katika shughuli zote za biashara
- Tunatii sheria zote husika na Kanuni, pamoja na sera na taratibu za KBR
- Tunaripoti kwa wakati matukio yoyote ya ukiukaji wa Kanuni kwa meneja, Kitengo cha Usimamizi wa Wafanyakazi (Rasilimali Watu), Idara ya Sheria, Timu ya Maadili ya Biashara au Huduma ya Dharura ya Maadili katika www.ethics.kbr.com
- Tunaomba ushauri kwa meneja au Idara ya Sheria tukikabiliwa na changamoto kuhusu suala la kimaadili au kisheria, au kuwasiliana na Huduma ya Dharura ya Maadili, ambapo tunaweza kuuliza maswali chini ya kipengele cha Kidhibiti Maswali (Question Manager)

**Wasimamizi wana majukumu ya ziada. Haya yanajumuisha:**

- Kuwa kielelezo cha tabia ya uadilifu
- Kukuza utamaduni wa kimaadili na maamuzi ya uadilifu
- Kuhimiza mawasiliano ya wazi na kuunda mazingira ambapo wafanyakazi wako huru kuripoti masuala
- Kutoa ushauri na maoni kuhusu maswali na masuala husika
- Kujua wakati wa kuripoti matukio ya ukiukaji, kuripoti masuala kwa usimamizi au kutafuta msaada kutoka kwa wataalamu wa kampuni
- Kuhakikisha kwamba hakuna kulipiza kisasi kwa mfanyakazi yeyote anayeripoti matukio ya uwezekano wa ukiukaji wa Kanuni au sheria

# Jinsi Tunavyofanya Maamuzi

Kufanya kitu kinachofaa si rahisi au wazi kila wakati. Kanuni ni zana muhimu, lakini haziwezi kutoa mwongozo katika kila hali. Kwa hivyo, maamuzi ya biashara yanapaswa kufanywa kwa uadilifu kila wakati.



**Bofya majibu yaliyo hapa chini ya kukuongoza kufanya maamuzi ya uadilifu.**

**Je, kitendo hiki kinaweza kukiuka sheria au kanuni zozote?**

NDIYO | HAPANA

**Je, kitendo hiki kinalingana na Kanuni, sera na taratibu zetu?**

NDIYO | HAPANA

**Je, kitendo hiki kinalingana na maadili ya KBR na kitaendeleza dhamira yetu na kuimarisha sifa yetu?**

NDIYO | HAPANA

**Je, kitendo hiki kinaweza kudhuru mahusiano yetu na wateja au washirika wa biashara?**

NDIYO | HAPANA

**Ikiwa kitendo hiki kitafichuliwa, itaonekana kwamba nilitenda kwa uadilifu? Je, nitafurahia ikiwa kitendo hiki kitafichuliwa hadharani?**

NDIYO | HAPANA

# Jinsi Tunavyoomba Msaada, Kuripoti na Kuuliza Maswali



Kama watu waadilifu, tuna wajibu wa kuripoti kitendo chochote kinachoshukiwa kukiuka Kanuni, na tunatarajia wafanyakazi na watu wengine kuripoti tabia na matendo yasiyo adilifu ambayo hayafuati Kanuni zetu. Hii inamaanisha kuripoti masuala yetu hata kama hatuna uhakika kwamba tuna maelezo yote. Mara nyingi, tunaweza kuripoti masuala yetu kwa meneja, ambaye anaweza kutusaidia kujadili hatua bora ya kuchukua.

Huduma ya Dharura ya Maadili ya KBR inasimamiwa na kampuni huru. Inapatikana wakati wowote, mchana na usiku, wiki nzima, kwa lugha nyingi. Huduma ya Dharura ya Maadili inaweza kutumiwa na mtu yeyote wa ndani au nje ya KBR kuwasilisha ripoti ya siri.

Huduma ya Dharura ya Maadili ina kipengele cha "Kidhibiti Maswali" ambapo tunaweza kuuliza maswali au kuomba ufafanuzi kuhusu masuala ya utiifu na kimaadili kutoka kwa Timu ya Maadili ya Biashara. Jinsi zilivyo ripoti za matukio ya uwezekano wa ukiukaji wa kanuni, unaweza kuwasilisha maswali au masuala kwa Huduma ya Dharura ya Maadili bila kujitambulisha.

**Katika KBR, unaweza kuwasiliana na:**

- Huduma ya Dharura ya Maadili (ina chaguo la kuficha utambulisho)
  - Wavuti:
    - www.ethics.kbr.com
  - Piga simu:
    - Marekani: (800) 461-9330
    - Uingereza: 0808 189 1053
    - Kwa nambari za simu katika nchi nyingine zote, tembelea www.ethics.kbr.com
  - Tuma neno "Ripoti" kwa nambari 832-479-1340 (Inapatikana Marekani pekee)
- Mkurugenzi wa Maadili ya Biashara katika fhoukbrcode@kbr.com
- Timu ya Maadili ya Biashara kwa barua:
  - P.O. Box 2464, Houston, TX 77252-2464 USA
- Mwakilishi anayefaa wa Idara ya Sheria; Huduma ya Ukaguzi (Audit Services); Kitengo cha Usimamizi wa Wafanyakazi (Raslimali Watu); Afya, Usalama, Ulinzi na Mazingira ya KBR; au idara nyingine inayohusiana na masuala ya utiifu
- Msimamizi au meneja wako
- Mwanachama wa Timu ya Usimamizi Mkuu (Executive Leadership Team)

**Pata Maelezo Zaidi**
Maswali Yanayoulizwa Sana (FAQs) kuhusu Kuripoti

## Tunaheshimu Usiri na Kuficha Utambulisho

Unaweza kuripoti masuala au matukio yanayoshukiwa kukiuka Kanuni kwa usiri au bila kujitambulisha. Ripoti za siri zinaweza kuwasilishwa kwa Huduma ya Dharura ya Maadili inayosimamiwa na kampuni huru. Ukiwasilisha ripoti ya siri kupitia Huduma ya Dharura ya Maadili, KBR haitakutambua, lakini itaweza kuwasiliana nawe mara kwa mara kupitia mfumo wa kutuma ujumbe. Ikiwa utaamua kuficha utambulisho, tunaomba utoe maelezo ya kweli na ya kutosha ili tuweze kufuatilia suala lako ipasavyo.

## Hatukubali Kulipiza Kisasi

Uadilifu unatutaka turipoti. Hatulipizi kisasi kamwe dhidi ya watu wanaowasilisha masuala kwa nia njema. Wafanyakazi na timu zetu zinategemea uwazi na uaminifu ili kufanya kazi yao bora zaidi. Hatuwezi kukuza maadili hayo katika mazingira ya vitisho au athari nyingine mbaya. Tabia hiyo haikubaliwi katika mazingira yetu ya kazi, na tunashirikiana kikamilifu na huduma zozote za upelelezi au uchunguzi kuhusu madai ya kutekelezwa kwa matendo mabaya.

KBR haikubali kulipiza kisasi kwa kuripoti tukio la uwezekano wa ukiukaji wa Kanuni au sheria. KBR inatarajia ripoti hizo kuwasilishwa kwa nia njema. Hii haimaanishi kwamba anayeripoti lazima awe na maelezo yote; anayeripoti anapaswa kuwa huru kuuliza maswali na kuripoti suala lolote linalosababisha wasiwasi bila kuogopa kulipiza kisasi. Hata hivyo, ripoti zinazojulikana kwa uwazi kuwa ni za uongo au za nia mbaya, hazijawasilishwa kwa nia njema na zinaweza kusababisha kuchukuliwa hatua ya kinidhamu.

Ulipizaji kisasi ambao hauruhusiwi unaweza kujumuisha unyanyasaji au kutishia wafanyakazi na watu wengine wanaoripoti madai ya kutekelezwa kwa matendo mabaya au kuwahimiza wengine kuripoti. Tabia ya kulipiza kisasi ya namna yoyote, majaribio ya kukataza mtu kuripoti, na kutoripoti matendo mabaya hailingani na maadili yetu na inaweza kusababisha kuchukuliwa hatua ya kinidhamu, ikijumuisha kufutwa kazi.

Hakuna chochote katika Kanuni hizi kinachowazuia wafanyakazi kutekeleza haki zao za kisheria au wajibu wa kuripoti matukio ya uwezekano wa ukiukaji wa sheria kwa mamlaka husika za serikali wakati wowote, bila kuripoti suala husika kwa, au kuomba idhini mapema kutoka kwa Kampuni.






# Kuthamini Kila Mmoja Wetu

- Tunadumisha Afya na Usalama wa Wafanyakazi na Makontrakta Wetu
- Tunahimiza Mazingira ya Heshima Kazini

# Tunadumisha Afya na Usalama wa Wafanyakazi na Makontrakta Wetu

ZERO HARM
COURAGE TO CARE

Mafanikio ya biashara ya KBR yanategemea uwezo wake wa kuendelea kuimarisha ubora wa huduma tunazotoa, huku pia tukilinda afya, usalama na ulinzi wa wale wanaofanya kazi moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja na kampuni. Tunahitaji kujitolea na uwajibikaji katika kudumisha afya, usalama, ulinzi na mazingira (HSSE, Health, Safety, Security and Enviroment) kutoka kwa wafanyakazi na makontrakta wote. Wajibu huu unalenga maslahi bora ya wateja, wafanyakazi, makontrakta, wadau na jamii zetu ambapo tunaishi na kufanya kazi.

## Jinsi Tunavyodumisha Afya na Usalama wa Wafanyakazi na Makontrakta Wetu

- Kulinda na kujitahidi kuboresha afya, usalama na ulinzi wa wafanyakazi na makontrakta wetu kila wakati
- Kukomesha matukio kupitia utamaduni wa Kuzuia Madhara Kabisa (Zero Harm)
- Kutimiza masharti maalum ya wateja na kuhakikisha wateja wanaendelea kuridhishwa
- Kuweka malengo ya HSSE, kupima matokeo na kukadiria na kuendelea kuboresha taratibu na huduma kupitia matumizi ya mfumo bora wa usimamizi
- Usimamizi wa moja kwa moja unapaswa kuchukua jukumu la uongozi katika mawasiliano, utekelezaji na utiifu wa sera na taratibu za HSSE
- Kutumia ujuzi wa kiufundi kwenye sehemu zote za HSSE za uhandisi na usanifu
- Kuwasiliana kwa uwazi na wadau na kuhakikisha wanaelewa sera, mpango na taratibu za HSSE
- Kutambua utendaji bora wa HSSE

### Kuzuia Madhara Kabisa na Ujasiri wa Kuwajali Wengine (Courage to Care)

Katika KBR, tunaamini kwamba tunaweza kufanikisha hatua ya Kuzuia Madhara Kabisa. Tunaamini kwamba matukio yote ya kazini yanaweza kuzuiwa. Sera yetu ya Mchakato wa Mazungumzo ya Ujasiri wa Kuwajali Wengine (Courage to Care Conversation Process) ni muhimu katika kuendelea kukuza ufahamu wa vitendo visivyo salama kupitia utazamaji, uchukuaji wa hatua na mazungumzo. Lengo la sera ya Mchakato wa Mazungumzo ya Ujasiri wa Kuwajali Wengine ni kuendelea kutathmini mazingira ya kazi na kuangazia watu na vitendo vyao.

Vitendo visivyo salama ni tabia mahususi zinazoweza kusababisha kisa fulani. Baada ya kuona kitendo kisicho salama, sera ya Mchakato wa Mazungumzo ya Ujasiri wa Kuwajali Wengine inahitaji aliyeona achukue hatua mara moja, si tu kurekebisha kitendo hicho kisicho salama, lakini pia kueleza kiwango chake cha usalama wa binafsi. Hii inasababisha kufahamu hatari na zaidi kujitolea kudumisha usalama kwa watu walioona na kushiriki katika kitendo kisicho salama.

**Pata Maelezo Zaidi**

Global HSSE

# Tunahimiza Mazingira ya Heshima Kazini

Kwa sababu wafanyakazi wetu ni kiini cha kila kitu tunachofanya, tunaamini kuwa wafanyakazi wote wanapaswa kupewa heshima. Hii inamaanisha kukubali michango ya kila mmoja kulingana na ustahiki na kumpa kila mtu fursa sawa za kuchangia na kufaulu katika KBR. Hatukubali unyanyasaji au ubaguzi wa namna yoyote. Ili kuziwezesha timu zetu kufanya kazi bora, tunadumisha mazingira ya kazi ambapo haki na uwezo wa kila mtu unaheshimiwa.

## Jinsi Tunavyohimiza Mazingira ya Heshima Kazini

- Kuheshimu wengine kila wakati, iwe tunashirikiana na wanatimu, wateja wetu au washirika wetu wa biashara
- Kuzingatia jinsi vitendo na maneno yetu yanavyoweza kuchukuliwa na wengine
- Hatubagui au kushiriki katika vitendo vya unyanyasaji kulingana na yafuatayo:
  - Mbari
  - Rangi
  - Imani za dini
  - Utaifa au asili
  - Jinsia, ujauzito, mwelekeo wa kingono, jinsia, utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kijinsia au hali ya kubadilisha jinsia
  - Ulemavu wa mwili au akili
  - Umri
  - Hali ya uanajeshi au mwanajeshi aliyestaafu
  - Maelezo ya kijenetiki
  - Hali au sifa nyingine yoyote inayolindwa na sheria inayotumika
- Hatunyanyasi, kutishia au kuchokoza wengine kwa namna yoyote, ikijumuisha kwa kutumia kauli za kingono au za kuchochea mawazo ya ngono au kwa kutoa vitisho vya kusababisha vurugu, kufanya vitendo visivyofaa vya ajira au kuahadi kufanya vitendo vya mapendeleo ya ajira
- Kufanya maamuzi yote ya kuajiri wafanyakazi na kupandisha cheo kulingana ustahiki na haki
- Kuripoti ikiwa tutashuhudia au kugundua vitendo vya ubaguzi, unyanyasaji au ukosefu wa heshima katika mazingira yetu ya kazini





## Kuelewa Unyanyasaji

Ingawa vitendo vya unyanyasaji vinaweza kufanywa kimakusudi, si lazima iwe hivyo. Jambo muhimu ni jinsi inavyochukuliwa. Hatupaswi kufanya au kusema kitu ambacho wengine wanaweza kukichukulia kama cha kukera. Unyanyasaji unaweza kuwa kwa namna nyingi:

- Tunachosema au kuandika, kama vile maoni ya kukera au kudharau au maneno ya kuaibisha ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, yanayolenga mbari, kabila au jinsia ya mtu yeyote, pamoja na maoni au maombi ya kingono, au lugha ya kutishia au matusi
- Tunachofanya, ikiwa ni pamoja na miguso isiyofaa au kumzuia mtu kwa kusimama mbele yake
- Tunachoonyesha, kama vile picha za kingono au za kukera au tovuti zilizofunguliwa kwenye kompyuta ya ofisi
- Mawasiliano tunayofanya kupitia ujumbe wa kielektroniki au mitandao jamii

## Kutoa Majibu

**Swali** Niliajiriwa hivi karibuni kama mwanachama wa timu ya kukuza mikakati. Ili kutengenezewa mahali pangu pa kazi, nilifanya mkutano na msaidizi wa ndani wa idara ya TEHAMA (IT) anayeitwa Sam. Sam alipokuwa akinisaidia kuweka mipangilio ya kompyuta yangu, aliweka mkono wake kwenye paja langu. Sikusema kitu na Sam akamaliza kuweka mipangilio ya kompyuta yangu. Nimetulia kwa kuwa tukio hilo limepita, lakini sasa nina wasiwasi kuhusu kuwasiliana na idara ya TEHAMA ikiwa kuna chochote kinachohitaji kurekebishwa au kusasishwa. Je, ninapaswa kufanya nini?

**Jibu** Tabia ya Sam hairuhusiwi. Miguso isiyofaa hairuhusiwi katika mazingira ya kazi. Unapaswa kumwambia meneja wako, Kitengo cha Usimamizi wa Wafanyakazi (Rasilimali Watu) au Timu ya Maadili ya Biashara kuhusu hali yako, au ripoti kwa Huduma ya Dharura ya Maadili.

**Swali** Nimeanza kufanya kazi hivi karibuni tu katika KBR, na kwa ujumla, nina furaha sana. Kwa bahati mbaya, mmoja wa wafanyakazi wenzangu alinipa wasiwasi sana. Katika mkutano wangu wa kwanza, niligundua kwamba mmoja wa wafanyakazi wenzangu, anayeitwa Landon, alionekana akinikodolea macho. Baadaye siku hiyo, nilipokea barua pepe kutoka kwake. Kwenye barua pepe, aliniambia kwamba alipata anwani yangu ya barua pepe katika saraka ya kampuni kwa sababu aliona kuwa nilikuwa mrembo. Bila shaka, alipata akaunti zangu za Instagram na Facebook pia, kwa sababu nilipata maombi ya kuwa rafiki kutoka kwake kwenye akaunti zote mbili nilipofika nyumbani jioni hiyo. Nilipomwona siku iliyofuata, nilimwambia akome kunitumia ujumbe. Baada ya hapo, niligundua kwamba sijumuishwi kwenye mikutano kadhaa na kwamba kazi zangu zilikuwa zimepunguzwa. Sina uhakika iwapo masuala ya kazi yanahusiana na hilo. Je, ninapaswa kufanya nini?

**Jibu** Kwa sababu KBR inachukulia kwa uzito masuala ya unyanyasaji na kulipiza kisasi, unapaswa kujadili hali yako mara moja na meneja au Kitengo cha Usimamizi wa Wafanyakazi (Rasilimali Watu), au kuripoti suala hilo kwa Timu ya Maadili ya Biashara, Idara ya Sheria au Huduma ya Dharura ya Maadili. Suala hilo litashughulikiwa na uchunguzi utafanywa ili kubainisha ikiwa tukio la ukiukaji wa Kanuni au sera nyingine ya KBR lilifanyika.



# Kutoa Huduma kwa Uadilifu

- Tunazuia Ukinzani wa Maslahi
- Tunazuia Hongo na Ufisadi
- Tunatoa na Kupokea Zawadi za Kibiashara kwa Uwajibikaji
- Tunafanya Kazi na Biashara ya Kimataifa kwa Uadilifu
- Tunashindana kwa Haki
- Tunatenda Mambo kwa Ukweli

# Tunazuia Ukinzani wa Maslahi

Kama timu ya jumla, hatuweki maslahi ya binafsi mbele ya maslahi bora ya KBR. Tunatoa huduma bora wakati ambapo haturuhusu mahusiano ya binafsi au maslahi mengine kuathiri maamuzi yetu. Tunazingatia ukweli, uadilifu na uwazi tunaposhughulikia matukio halisi au yanayoweza kutokea ya ukinzani wa maslahi. Hata dalili tu ya tukio la ukinzani wa maslahi inaweza kusababisha hatari ya kuharibika kwa sifa ya KBR na kuathiri motisha ya wafanyakazi wetu.

## Jinsi Tunavyozuia Ukinzani wa Maslahi

- Kufanya maamuzi bila mapendeleo
- Kuzingatia zaidi hali, mahusiano au shughuli ambazo zinaweza kuathiri ujumla wetu
- Kuripoti haraka iwezekanavyo matukio yoyote yanayoweza kusababisha ukinzani wa maslahi kwa meneja, Idara ya Sheria au Timu ya Maadili ya Biashara; uwazi ni muhimu kwa matukio yanayoweza kusababisha ukinzani wa maslahi
- Kujiondoa kwenye maamuzi yanayohusisha matukio yetu binafsi yanayoweza kusababisha ukinzani wa maslahi
- Kutoshiriki katika maamuzi ya kuajiri au kufanya biashara na jamaa wetu wa karibu
- Kufichua maslahi ya kifedha ambayo yanaweza kutofautiana na maslahi ya KBR
- Kufuata taratibu zote za kuripoti zilizo mahususi kwa wanachama wa bodi, Afisa Mkuu Mtendaji na usimamizi mkuu ambao hukagua matumizi ya fedha au mali za KBR
- Kutumia taratibu za kusaidia kampuni kuepuka ukinzani wa maslahi ya kishirika

### Kuelewa Ukinzani wa Maslahi

Ukinzani wa maslahi unaweza kutokea wakati mahusiano au maslahi yetu binafsi yanatofautiana na maslahi bora ya KBR, hali ambayo yanaweza kuathiri hali yetu ya ujumla. Hii inaweza kuwa namna nyingi:

- Kuhudumu kama mkurugenzi au mshauri wa shirika lisilo la KBR
- Kuwa na hamu ya kunufaika kifedha kutoka kwa mshindani, mteja au muuzaji mtarajiwa
- Kushiriki katika miamala ya binafsi na wafanyakazi wengine, wauzaji au washirika wa biashara
- Kuwa na kazi ya pili ambayo inakinzana na maslahi ya KBR au inazuia utendaji wa kazi
- Kuajiri au kusimamia jamaa wako wa karibu
- Kufanya biashara ya KBR na muuzaji ambaye ni jamaa wako wa karibu
- Kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mfanyakazi mwenzako, hasa mfanyakazi unayemsimamia



### Watu Waadilifu

Kama watu waadilifu wanaothamini ukweli, tunajua hakuna haja ya kuficha tukio linaloweza kusababisha ukinzani wa maslahi. Meneja wako, Idara ya Sheria na Timu ya Maadili ya Biashara wote wanapatikana ili kutoa ushauri. Kumbuka kwamba hata dalili tu ya tukio la ukinzani wa maslahi inaweza kudhuru sifa yako na yetu. Fichua kila wakati matukio yanayoweza kusababisha ukinzani wa maslahi na utafute ushauri ikiwa huna uhakika.

# Kuchagua Uadilifu

Wakati mwingine fursa ya biashara inaweza kusababisha ukinzani wa maslahi. Fursa hiyo ya biashara inaweza kuwa yako peke yako, au inaweza kuwa ya KBR. Zingatia maswali yaliyo upande wa kulia ya kukusaidia kubainisha ikiwa kuna uwezekano wa ukinzani wa maslahi.

## Kutoa Majibu

**Swali** Nimekuwa mhandisi katika KBR kwa miaka kumi na mbili. Timu yangu imefanikiwa kupitisha lengo kuu lililowekwa, na ningependa kuwapa zawadi. Ninafikiri kushiriki chakula cha jioni kama timu kutafaa zaidi. Ndugu yangu anamiliki hoteli na anaweza kuhudumia watu wengi. Je, ninaweza kuzungumza naye kuhusu kutuandalia chakula chetu cha jioni?

**Jibu** Hapana. Hii inaweza kusababisha ukinzani wa maslahi. Hatuwezi kutumia cheo chetu katika KBR kufanya biashara na mwanafamilia, hata kama biashara ya mwanafamilia huyo haishindani na yetu. Unaweza kujadili hali yako na meneja wako au Idara ya Sheria. Ukijiondoa kwenye maamuzi yoyote kuhusu biashara ya mwanafamilia, KBR inaweza kuzingatia kutumia huduma zake za hoteli kwa matukio ya siku za usoni.

**Pata Maelezo Zaidi**

Fomu ya Biashara ya Nje na Ukinzani wa Maslahi

**Bofya jibu la kila maswali yaliyo hapa chini ya kukusaidia kubainisha ikiwa kuna tukio linaloweza kusababisha ukinzani wa maslahi.**

**Je, fursa hiyo ya biashara ya binafsi inahusisha muuzaji, mshindani au mshirika wa biashara wa KBR, au ni aina ya biashara inayofanana na biashara ya KBR?**

NDIYO | HAPANA

**Je, fursa hiyo ya biashara ya binafsi itapunguza au kuathiri uwezo wako wa kutekeleza majukumu yako ya kazi katika KBR?**

NDIYO | HAPANA

**Je, fursa hiyo ya biashara ya binafsi itaathiri uwezo wako kufanya maamuzi ya biashara bila mapendeleo kwa niaba ya KBR au kukusababisha ushindane na KBR?**

NDIYO | HAPANA

**Je, mwanafamilia anahusika katika kutoa huduma hiyo kwa KBR?**

NDIYO | HAPANA

**Je, utatatizika kufanya uamuzi wa biashara bila mapendeleo kwa niaba ya KBR, au itaonekana kwa wengine kwamba uamuzi wowote ulikuwa na mapendeleo?**

NDIYO | HAPANA

# Tunazuia Hongo na Ufisadi

Tunapokuza na kudumisha mahusiano ya biashara, tunatoa huduma bora kila wakati kwa uadilifu. Haturuhusu kutoa au kupokea hongo au malipo yasiyofaa katika hali zozote. Ufisadi hudhuru jamii za mahali ambapo tunafanya biashara na unaweza kusababisha kupigwa faini na hata kufungwa jela. Unaweza pia kuharibu sifa yetu. Bila kujali desturi au sheria, popote tunapofanya biashara duniani, hatulegezi kamwe maadili yetu. Tunapoendelea kukua, msimamo wetu wa uadilifu hautabadilika.

## Jinsi Tunavyozuia Hongo na Ufisadi

- Kutoahidi, kutoa, kuidhinisha au kukubali malipo yasiyofaa, ikijumuisha bahashishi, hongo au mlungula
- Kutahadhari zaidi kuhusu malipo yasiyofaa tunapofanya kazi na wafanyakazi wa serikali
- Kufanya uchunguzi wa msingi wa hatari unaofaa kuhusu washirika wa biashara watarajiwa, ikijumuisha mashirika ya serikali, kabla ya kushirikiana
- Kutotumia mshirika mwingine kufanya malipo ambayo sisi wenyewe hatuwezi kuyafanya
- Kuripoti haraka iwezekanavyo masuala yoyote kuhusu malipo ambayo huenda hayafai
- Kutotekeleza malipo ya huduma au uharakishaji, kwa mfanyakazi au ofisa wa serikali ili kuharakisha au kupendelewa katika mchakato wa kawaida wa hatua ya serikali inayolipiwa
- Kufuata sera na taratibu zote za kupinga ufisadi za KBR, hasa kuhusu masharti ya uidhinishaji na kupata vyeti vya kufanya miamala fulani



### Hongo au Malipo Yasiyofaa Ni Nini?

Hongo au malipo yasiyofaa ni kuahidi, kutoa au kupokea pesa, zawadi au kitu chochote cha thamani moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili kumshawishi mtu kufanya kitu kisichofaa, haramu, kinachokiuka jukumu lake au ili kupendelewa.

Hongo na malipo yasiyofaa yanaweza kuwa kwa namna nyingi na inaweza kujumuisha vitu vya kushika (zawadi) na vitu visivyo vya kushika (ahadi) zaidi ya pesa. Malipo yasiyofaa yanaweza kujitokeza wakati unashirikiana na maofisa wa kigeni, kwenye kandarasi za serikali au katika biashara. Ikiwa huna uhakika iwapo malipo yasiyofaa yanaweza kuwa yamehusika, ripoti suala lako kwa mfanyakazi wa Idara ya Sheria — ikijumuisha Timu ya Utiifu wa Sera ya Kupinga Ufisadi (Anti-Corruption Compliance) na Timu ya Maadili ya Biashara — au Huduma ya Dharura ya Maadili.


**Pata Maelezo Zaidi**

Anti-Corruption Compliance

Anti-Corruption Procedures

# Kuchagua Uadilifu

Bofya kila duara ili upate maelezo kuhusu aina tofauti za malipo yasiyofaa.






# Tunatoa na Kupokea Zawadi za Kibiashara kwa Kuwajibika

Kama washirika wa kuaminika kwa wateja wetu, hatutoi au kupokea zawadi au vitu vingine vya hisani ili kushawishi uamuzi wa biashara. Hata dalili tu ya kuonyesha ushawishi inaweza kudhuru sifa yetu. Ingawa wakati mwingine tunaweza kutoa au kupokea zawadi kama sehemu ya kawaida ya kufanya biashara na kukuza mahusiano, haturuhusu zawadi hizo kuathiri uamuzi wetu wa biashara. Mafanikio yetu yamejikita katika msingi wa huduma bora tunayotoa kupitia kwa wafanyakazi wetu, uadilifu wetu na suluhu zetu bunifu. Hatutoi au kukubali zawadi zisizofaa.

## Jinsi Tunavyotoa na Kupokea Zawadi za Kibiashara kwa Uwajibikaji

- Kutotoa au kukubali vitu vya hisani vya thamani kubwa au vya mara kwa mara (k.m., zawadi, makaribisho, usafiri au burudani) kwa au kutoka kwa washirika wengine
- Kutotoa au kukubali pesa taslimu au vitu vinavyolingana na thamani ya pesa taslimu, ikijumuisha kadi za zawadi
- Kutoomba zawadi kutoka kwa washirika wengine
- Kutokubali zawadi kutoka kwa muuzaji au muuzaji mtarajiwa tunayemtathmini kwa sasa au ambaye tunashauriana naye kwa sababu hiyo inaweza kuonyesha picha mbaya
- Kutii Taratibu za Kupinga Ufisadi za KBR, ambazo zinabainisha hali ambapo zawadi, makaribisho, usafiri au burudani zinaweza kutolewa au kupokelewa, ikijumuisha wakati ambapo tunaweza kutoa zawadi kwa maofisa na wafanyakazi wa serikali

### Zawadi za Kawaida na Zinazofaa

Vyakula vya kibiashara, burudani na zawadi za kawaida na zinazofaa zinaweza kutolewa au kupokelewa mradi zawadi hiyo iliyotolewa au kupokelewa haionyeshi picha mbaya na inalingana na taratibu zetu. Shughuli zote kama hizo lazima ziripotiwe, kuidhinishwa na kutekelezwa kulingana na taratibu zetu. Ikiwa hakuna utaratibu maalum, zawadi hiyo inapaswa kuripotiwa kwa, na kuidhinishwa mapema na msimamizi.

### Kutoa Majibu

**Swali** Ninafanya kazi katika idara ya manunuzi. Je, ninaruhusiwa kukubali mwaliko wa chakula cha mchana cha kibiashara kutoka kwa muuzaji fulani?

**Jibu** Inategemea. Chakula cha mchana cha kibiashara kinaweza kuwa zawadi ya kawaida na inayofaa. Hata hivyo, kulingana na jukumu lako katika idara ya manunuzi, ambapo una uwezo wa kushawishi utoaji wa kandarasi, lazima uwe makini zaidi. Pata idhini mapema kila wakati na ufuate taratibu za malipo ya fidia.

Masharti ya kisheria kuhusu zawadi za kibiashara yanaweza kuwa makali zaidi kwa kandarasi za serikali kuliko kandarasi za biashara. Lazima tufuate masharti hayo tunaposhughulika na kandarasi za serikali.

# Tunafanya Kazi na Biashara ya Kimataifa kwa Uadilifu



KBR inazingatia viwango vya juu vya uadilifu popote tunapofanya biashara, duniani kote. Kufanya biashara ya kimataifa kwa uadilifu kunatusaidia tunapojitahidi kuunda ulimwengu bora na salama zaidi. Hatukiuki kamwe sheria za biashara za kimataifa, ambazo zinajumuisha sheria za uingizaji na utoaji wa bidhaa nchini, pamoja na vizuizi na vikwazo vya kiuchumi. Sheria hizi zinaweza kutofautiana kulingana na eneo, na tuna wajibu wa kuzijua na kuzifuata. Kutozitii kunaweza kusababisha madhara makubwa ya sifa, kupigwa faini na hata kufungwa jela.

## Jinsi Tunavyofanya Kazi na Biashara ya Kimataifa kwa Uadilifu

- Kutofanya biashara nje ya nchi bila kwanza kujua sheria na kanuni za biashara
- Kutii sheria na kanuni zote za biashara
- Kubaini ikiwa hatua ya kushiriki data ya kiufundi na mtu mgeni itasababisha kuchukuliwa kwamba ni mauzo ya nje ya nchi
- Kuhakikisha kwamba tumepata leseni zozote zinazohitajika za mauzo ya nje ya nchi, leseni za uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi na vibali vingine
- Kutii kanuni zote za kupinga ususiaji za Marekani
- Kutii vizuizi na vikwazo vingine vyote vya biashara vilivyowekwa na Ofisi ya Udhibiti wa Raslimali za Kigeni (OFAC, Office of Foreign Assets Control) vya Idara ya Hazina ya Marekani (U.S. Department of the Treasury) na mamlaka za serikali za kuweka vikwazo za mataifa mengine
- Kuwasiliana na Ofisi ya Utiifu wa Sheria za Biashara ya Kimataifa (ITCO, International Trade Compliance Office) ya Idara ya Sheria ya KBR ili kupata ushauri kuhusu masuala yote yanayohusiana na biashara
- Kufuata sera na taratibu zote za KBR zinazohusiana na biashara ya kimataifa

**Pata Maelezo Zaidi**
Export Compliance Manual
International Trade Compliance Office

# Tunashindana kwa Haki

Tunatoa bidhaa zinazowasaidia wateja wetu duniani kote ili kutimiza malengo yao muhimu zaidi, na tunafaulu katika kazi zetu kwa njia ya haki. Ushindani wa wazi na haki unatusukuma kuwa bora zaidi, na kutuwezesha kuwa wabunifu. Hatutafuti mbinu za ushindani usio wa haki sokoni. Hii haitadhuru tu mahusiano yetu na wateja wetu na washirika wa biashara, lakini inaweza pia kusababisha kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

## Jinsi Tunavyoshindana Kwa Haki

- Kutii sheria zote zinazohusika za ushindani na kupinga ushindani usio wa haki
- Kutofanya mazungumzo au kuingia katika mkataba na mshindani kuhusu:
    - Bei
    - Sheria na masharti ya huduma au mauzo
    - Usambazaji
    - Maeneo
    - Wateja
- Kutafuta ushauri kutoka kwa Idara ya Sheria ya KBR kabla ya kushiriki katika mazungumzo ya kubadilishana maelezo na washindani kupitia miungano ya biashara au mikutano ya kisekta
- Kutotoa madai ya uongo kuhusu huduma au bidhaa za washindani
- Kuripoti haraka iwezekanavyo kwa Idara ya Sheria ya KBR majaribio yoyote ya washindani ya kuingia katika mkataba usio halali au maelezo yoyote ya bei au zabuni tunayapokea kutoka kwa mshindani




### Kutoa Majibu

**Swali** Ninafanya kazi katika idara ya Kuendeleza Biashara (Business Development). Katika maonyesho ya hivi karibuni ya biashara, nilikutana na mfanyakazi mwenzangu wa zamani ambaye sasa anafanyia kazi mshindani wetu. Alinialika nijiunge katika mkutano tofauti na kikundi cha sekta ambacho kinataka kubadilishana maelezo kuhusu taratibu za biashara na takwimu za utendaji kwa madhumuni ya kuweka viwango vya ulinganishaji. Je, ninaweza kuhudhuria mkutano huo?

**Jibu** Kushiriki maelezo ya KBR na washindani kunaweza kukiuka sheria za kupinga ushindani usio wa haki, hata kama kusudi lake ni kubainisha viwango vya kisekta. Pata ushauri kutoka kwa Idara ya Sheria kabla ya kuamua kuhudhuria.

# Tunatenda kwa Ukweli

Hatuogopi kukabiliana na changamoto zozote ana kwa ana, lakini tunafanya hivyo kwa ukweli. Tunajenga na kudumisha uaminifu kwa wateja wetu na washirika wa biashara kwa kuwakilisha KBR kwa ukweli. Kama wafanyakazi, pia tuna uwezo wa kufikia raslimali ambazo KBR imekusanya katika historia yake ndefu. Tunatumia raslimali na nyenzo hizi kwa madhumuni ya biashara pekee. Matumizi yoyote mabaya au ya kilaghai ya raslimali zetu yanahujumu uwezo wetu wa kuwa bora zaidi.

## Jinsi Tunavyotenda kwa Ukweli

- Kutoa maelezo ya ukweli kuhusu bidhaa na huduma zetu katika nyenzo zote za matangazo
- Kutopotosha au kutoa maelezo yasiyo ya kweli kuhusu bidhaa na huduma tunapojadiliana na wateja na washirika wa biashara
- Kukadiria vipindi vyote vya utekelezaji kwa usahihi, na kuelezea mabadiliko kwa ukweli
- Kutodharau washindani tunapoangazia bidhaa zetu
- Kutumia raslimali za KBR, ikijumuisha fedha, kwa madhumuni ya biashara pekee
- Kutotumia vibaya fedha au raslimali nyingine za KBR
- Kuripoti gharama na saa tulizofanya kazi kwa uaminifu na kwa usahihi


## Kutoa Majibu

**Swali** Baada ya muda, nimekuza urafiki mzuri na msimamizi wangu wa mauzo, George. Tulienda kujivinjari pamoja wikendi iliyopita na wanandoa wetu na tukafurahia zaidi. Hata hivyo, niligundua kwamba George alitumia kadi yake ya mikopo ya kampuni kulipia vyakula vyetu. Nilimwuliza kuhusu jambo hilo baadaye, na alisema kwamba nisijali. Bado sijihisi huru kwa sababu sina uhakika iwapo hilo lilikuwa tukio la matumizi mabaya ya fedha za kampuni. Je, lilikuwa ni tukio la matumizi mabaya?

**Jibu** Msimamizi wako hakupaswa kutumia kadi ya kampuni kulipia gharama za binafsi. Kuwasilisha gharama za uongo ni ulaghai na hakuruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni hizi. Kwa sababu George ni msimamizi wako, unapaswa kutumia Huduma ya Dharura ya Maadili kuripoti suala hilo.

**Swali** Kama mhandisi aliyekabidhiwa mradi wa utafiti, mimi huripoti kila wakati saa zangu za kazi kwa usahihi na kwenye msimbo unaofaa wa mradi. Hivi karibuni, meneja wangu aliniomba niripoti saa zangu za kazi kwenye msimbo tofauti wa mradi, hata kama unaonekana kuwa ni wa mradi ambao sikuushughulikia. Siko tayari kuripoti saa zangu kwenye msimbo wa mradi mwingine. Je, ninapaswa kufanya nini?

**Jibu** Unapaswa kuomba ufafanuzi kutoka kwa meneja wako. Mara nyingi kuna misimbo kadhaa ya mradi inayotumika kwa mradi mmoja, na mteja anaweza kupendelea msimbo mwingine wa mradi. Hata hivyo, ikiwa unashuku kwamba unaombwa kuripoti saa za kazi kwa mradi ambao haushughulikii, unapaswa kuripoti suala hilo kwa mkuu wa idara/mradi, Kitengo cha Usimamizi wa Wafanyakazi (Rasilimali Watu), Idara ya Sheria, Timu ya Maadili ya Biashara au Huduma ya Dharura ya Maadili.



# Kuthamini Raslimali Zetu Muhimu

- Tunalinda Faragha na Maelezo ya Binafsi
- Tunalinda Sifa Yetu
- Tunalinda Maelezo ya Siri na ya Kampuni
- Tunazuia Biashara za Kindani

# Tunalinda Faragha na Maelezo ya Binafsi

Kama kampuni kubwa ya kimataifa, tunakusanya maelezo ya binafsi kutoka kwa wafanyakazi na wateja katika harakati za kufanya kazi. Tunapolinda maelezo na haki za faragha za wadau wetu, tunaonyesha kwamba tunawathamini. Pia, tunapata na kudumisha uaminifu wao, jambo ambalo ni nguzo kuu ya mafanikio yetu endelevu. Tunalinda maelezo ya binafsi na data ambayo ni muhimu kwa ustawi wetu. Mbinu zetu za ulinzi wa usalama za safu nyingi hulinda rasilimali za maelezo na kuhakikisha faragha na usalama wa maelezo ya binafsi na ya biashara ya wadau wetu wote kulingana na sheria zinazohusika.

## Jinsi Tunavyolinda Faragha na Maelezo ya Binafsi

- Kuhakikisha kuwa watumiaji walioidhinishwa pekee ndio wanaweza kufikia mifumo yetu ya maelezo
- Kuwapa wafanyakazi uwezo wa kufikia tu data inayohitajika kwa kazi zao
- Kuhakikisha kwamba data ya KBR inahifadhiwa tu kwenye vifaa salama vilivyoidhinishwa na KBR
- Kutofungua viungo au viambatisho vya barua pepe vinavyotiliwa shaka
- Kukusanya na kulinda usalama wa maelezo yanayoweza kumtambulisha mtu pekee (PII, Personally Identifiable Information) yanayohitajika kwa madhumuni ya biashara
- Kufuata sera na taratibu zote za faragha na ulinzi wa data

## Maelezo ya Binafsi

Maelezo ya binafsi yanaweza kuwa kwa namna nyingi. Baadhi ya mifano ni:

- Jina kamili
- Nambari ya Ustawi wa Jamii
- Nambari ya leseni ya udereva
- Nambari ya kadi ya mikopo
- Anwani ya nyumbani
- Anwani ya barua pepe ya binafsi
- Nambari ya simu ya binafsi

Maelezo ya binafsi yanajumuisha sehemu kamili za maelezo ambazo zinaweza kumtambulisha mtu binafsi. Hata hivyo, aina nyingine za maelezo, zikijumuishwa, zinaweza pia kuwa maelezo ya binafsi yanapotumiwa kumtambulisha mtu binafsi. Baadhi ya aina hizi nyingine za maelezo ni:

- Tarehe na mahali pa kuzaliwa
- Nambari ya simu ya kazi au ya biashara
- Maelezo ya matibabu
- Maelezo ya elimu
- Mbari na dini

Fahamu aina hizi zote za maelezo na uhakikishe umeyalinda kwa usalama.

## Mfumo Wetu wa Mawasiliano

KBR inahifadhi data nyingi kwenye mfumo wake wa mawasiliano, ikijumuisha data ya binafsi. Kompyuta, seva, vifaa vya mkononi, programu na teknolojia nyingine zinatusaidia kufanikisha malengo mengi mbalimbali ya biashara. Tunapolinda mfumo huu, tunalinda pia data yote iliyomo.

Tunadumisha ulinzi na usalama wa mifumo yetu yote ya mawasiliano kila wakati. Hii inamaanisha kurekebisha au kubadilisha vifaa ambavyo vimepitwa na wakati au kuharibika, kuweka masasisho yote yanayohusiana na usalama, kutumia manenosiri magumu na mbinu nyingine za usalama za ndani na nje ya kampuni, na kufuata taratibu zote za kuhamisha na kufuta data.

**Pata Maelezo Zaidi**
Global Data Privacy Policy
Data Privacy and GDPR

# Tunalinda Sifa Yetu

Kwa zaidi ya miaka mia moja iliyopita, KBR imejenga sifa kutokana na suluhu na teknolojia bunifu. Ili kulinda sifa hiyo na mahusiano yetu ya biashara, tunawasiliana kama timu moja. Wadau wetu wana haki ya kupata maelezo ya ukweli na yasiyobadilika kuhusu KBR, na wasemaji wetu walioteuliwa wanahakikisha kuwa tunaweza kufanikisha hilo. Pia, sisi huwa makini kila wakati tunapotaja KBR kwenye mitandao jamii.

## Jinsi Tunavyolinda Sifa Yetu

- Kuelekeza maswali ya nje kwa mhudumu anayefaa
- Kutowakilisha mitazamo yetu binafsi kuwa mitazamo ya KBR kwenye mitandao jamii au kwenye mawasiliano mengine yoyote
- Kujitambulisha kama wafanyakazi wa KBR ikiwa tunatangaza bidhaa au huduma zetu
- Kufuata Kanuni na sera nyingine za kampuni tunapotumia mitandao jamii kwa madhumuni ya biashara au tunapotoa maoni kuhusu kampuni tunapotumia akaunti za binafsi au za biashara
- Kufuata Sera ya KBR kuhusu Mitandao Jamii



### Matumizi ya Mitandao Jamii

Mitandao jamii ni zana muhimu zaidi kwa mawasiliano ya moja kwa moja, kukusanya maelezo na kukuza miunganisho. Tunatumia mitandao jamii kushiriki ujumbe na maono yetu na kuendelea kuwafahamisha wengine kuhusu michango na bidhaa zetu bunifu.

Tunajua pia kwamba mawasiliano ya mtandaoni yanaweza kuwa mazuri na mabaya. Sisi huwa waangalifu sana kuhusu maudhui tunayochapisha kuhusu KBR. Hatukosei kamwe katika tunachochapisha, wala hatushiriki maelezo ya siri au kutumia vinginevyo mitandao jamii kwa njia ambayo inaweza kukiuka Sera ya KBR kuhusu Mitandao Jamii.  Pia, mitandao jamii haipaswi kuathiri wajibu wetu katika KBR. Haturuhusu kamwe matumizi ya kibinafsi ya mitandao jamii kutuchanganya tukiwa kazini.

**Pata Maelezo Zaidi**
Social Media Policy

# Tunalinda Maelezo ya Siri na ya Kampuni

Maelezo yetu ya siri na ya kampuni, ikijumuisha mali ya uvumbuzi (IP, Intellectual Property), inatufanya tuwe wa kipekee. Tunajitofautisha na washindani wetu kupitia suluhu zetu mpya, na lazima tulinde ubunifu na maarifa yetu tuliyoyapata kwa jasho. Raslimali hizi za biashara zitatusaidia kuendelea kuhudumia wateja wetu na washirika wa biashara kadri tunapostawi.

Kama sehemu yetu ya kuajiri wafanyakazi katika KBR, tunaweza kufikia maelezo yetu ya siri au ya mshirika wa biashara, ikijumuisha maelezo ya binafsi ya wateja wetu. Hatutumii kamwe maelezo haya bila uangalifu. Kushiriki maelezo ya siri na ya kampuni bila idhini kunaweza kudhuru KBR na wateja wake au kuwasaidia washindani wetu.

## Jinsi Tunavyolinda Maelezo ya Siri na ya Kampuni

- Kutotumia maelezo ya siri na ya kampuni ya KBR au ya washirika wetu wa biashara, isipokuwa kama ilivyoidhinishwa
- Kutofichua maelezo ya siri na ya kampuni ya KBR, au ya washirika wetu wa biashara, bila kupata idhini mapema
- Kutobeba wala kutumia maelezo ya siri au ya binafsi ya KBR au ya washirika wetu wa biashara tunapoondoka katika KBR
- Kutotumia maelezo ya siri au ya kampuni kutoka kwenye kazi za awali tunapofanya kazi katika KBR
- Kufuata masharti yote ya hakimiliki, hataza na chapa za biashara za KBR, pamoja na za wengine
- Kufuata sheria na masharti yote ya leseni tunapotumia raslimali za washirika wengine kama vile programu ya biashara
- Kulinda usalama wa hati, data na vifaa vyote kwa kutumia kufuli na manenosiri magumu
- Kutojadili maelezo ya siri katika maeneo ya umma, kama vile kwenye lifti na mikahawani
- Kuhakikisha kwamba ni wafanyakazi walioidhinishwa pekee ndio wanaweza kuingia mahali pa kazi, na kusindikiza wageni wote
- Kutumia mbinu za usalama zinazofaa tunapofanya kazi nje ya ofisi, ikijumuisha tunapofanyia kazi nyumbani
- Kuripoti haraka iwezekanavyo matukio yoyote ya ufichuzi haramu wa data au ukiukaji wa usalama

Maelezo ya Kimkakati ya Biashara

Maelezo ya Kampuni

Mali ya Uvumbuzi

**Kuchagua Uadilifu**

Maelezo ya siri na ya binafsi yanaweza kuwa kwa namna nyingi. Bofya duara ili upate mifano.

Maelezo ya Matangazo

Maelezo ya Fedha Yasiyo ya Umma

**Pata Maelezo Zaidi**

Critical Assets Management

Data/Document Classification and Management of Proprietary Information

# Tunazuia Biashara za Kindani

Maelezo yetu ya kimkakati ya biashara hayapatikana mara moja kwa umma kila wakati. Kama kampuni ya umma, hatutumii au kushiriki maelezo muhimu kama hayo yasiyo ya umma kwa manufaa ya kibinafsi. Washirika wetu wa biashara wanatuamini pia kulinda maelezo yao, na hatuwezi kamwe kusaliti imani hiyo. Aina yoyote ya Biashara za Kindani, ikijumuisha "kudokezea" au kushiriki maelezo ya ndani, hairuhusiwi. Kufanya hivyo kunaweza kudhuru sifa yetu na kunaweza kusababisha kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

## Jinsi Tunavyozuia Biashara za Kindani

- Kutoshiriki maelezo ya ndani ya kampuni na mtu yeyote nje ya KBR, ikijumuisha familia na marafiki
- Kutonunua wala kuuza hisa katika KBR au kampuni nyingine yoyote tukiwa na maelezo ya ndani yasiyo ya umma
- Kushiriki tu maelezo ya ndani na wafanyakazi wanaohitaji kujua kwa madhumuni ya biashara
- Kutotoa "kidokezo" au kushiriki maelezo ya ndani na mtu fulani nje ya KBR ambaye anaweza kuyatumia kununua au kuuza hisa
- Kutojaribu kubadilisha bei ya hisa kwa hila kwa kueneza habari za uongo



## Maelezo ya Ndani

Maelezo muhimu yasiyo ya umma au maelezo ya ndani, yanaweza kuwa kwa namna nyingi. Maelezo mengi yasiyo ya umma yatatolewa kwa umma hatimaye. Ni maelezo "ya ndani" ikiwa bado hayajatolewa kwa umma. Ifuatayo ni mifano kadhaa:

- Maelezo kuhusu muungano au ununuzi wa biashara unaotarajiwa
- Migawo maalum ya faida
- Uzinduzi wa bidhaa mpya au maelezo yasiyo ya umma kuhusu miradi mipya
- Matokeo ya kifedha ya KBR
- Maelezo kuhusu kesi ya mahakamani inayoendelea
- Matokeo kutokana na uchunguzi au upelezi
- Maelezo muhimu yasiyo ya umma kuhusu kampuni zingine, ikijumuisha wateja wetu, ambayo tunaweza kuyafahamu kutokana na kazi zetu katika KBR




# Kutoa Huduma kwa Uwazi

- Tunafanya Kazi kwa Uadilifu na Uwazi na Wateja wa Serikali
- Tunafanya Kazi kwa Uadilifu na Wauzaji na Washirika Wengine
- Tunaweka Rekodi na Akaunti Sahihi

# Tunafanya Kazi kwa Uadilifu na Uwazi na Wateja wa Serikali

Tumebahatika kutoa huduma kwa serikali ya Marekani na serikali nyingine duniani. Tunaelewa kwamba kazi ya serikali inahusu kutii wajibu maalum na matakwa ya kisheria na kimaadili, na tunayakubali kabisa. Viwango vyetu vya juu vya uadilifu vinahusu wateja wetu wote, lakini tunazingatia zaidi kutii majukumu yanayolipwa kwa kutumia pesa za umma. KBR inatii kanuni na sheria zote zinazotumika zinazohusiana na kandarasi za serikali. Kutotii kanuni na sheria hizi kunaweza kuhatarisha kandarasi za sasa na za siku za usoni za serikali.

## Jinsi Tunavyofanya Kazi kwa Uadilifu na Uwazi na Wateja wa Serikali

- Kutimiza ahadi zetu zote kikamilifu
- Kushiriki kwa uwazi vipengele vyote vya kandarasi, ikijumuisha gharama na ratiba kama inavyohitajika
- Kudhibiti kandarasi ipasavyo na kutoa uangalizi wa kutosha kwa utendaji wa kazi
- Kutotoa kitu chochote cha thamani kwa maofisa wa serikali au wafanyakazi wa mashirika ya serikali kwa kukiuka kanuni na sheria zinazotumika
- Kuweka na kuwasilisha rekodi sahihi na za kweli, ikijumuisha kuripoti saa za kazi
- Kutowasilisha madai, taarifa au maelezo ya uongo kwa wateja au kuhusu hati zozote za serikali
- Kushiriki katika mafunzo yote yanayohitajika yanayohusiana na kandarasi za serikali
- Kufuata sheria, sera na taratibu zote za manunuzi ya serikali
- Kuhakikisha kuwa wafanyakazi, wauzaji na makontrakta wote wa KBR wanafahamu na wanafuata Kanuni za Maadili ya Biashara na Kanuni za Maadili ya Wauzaji



**Pata Maelezo Zaidi**

Contractor Code of Business Ethics and Conduct Compliance Policy



# Tunafanya Kazi kwa Uadilifu na Wauzaji na Wahusika Wengine

Tunawapa wadau wetu wote thamani ya kipekee ya kudumu. Ili kuhakikisha kuwa hatulegezi msimamo wa ahadi hii, tunafanya kazi na wauzaji na washirika wengine ambao wanafuata viwango vyetu vya juu. Tunatafuta thamani bora kila wakati tunapojenga na kudumisha mahusiano ya kibiashara, bila kulegeza msimamo wetu wa uadilifu. Ili kulinda sifa yetu ya ubora na uadilifu, tunatenda haki na kuwa makini tunapofanya kazi na wauzaji na washirika wengine.

## Jinsi Tunavyofanya Kazi kwa Uadilifu na Wauzaji na Washirika Wengine

- Kudumisha haki kwa wauzaji na washirika wengine wote, bila kujali thamani ya kibiashara ya uhusiano huo
- Kutafuta wauzaji na washirika wengine wanaofuata maadili yetu pamoja na kutusaidia kufanikisha malengo ya kibiashara
- Kuchagua wauzaji na washirika wengine kulingana na kigezo cha jumla, kama vile bei, ubora, upatikanaji na utendaji bora
- Kuwasiliana kwa uwazi na ukweli ili kutatua matatizo ya kibiashara yanayoweza kutokea
- Kuhakikisha kwamba wauzaji na washirika wengine ni waadilifu, wanafuata sheria na wanatii Kanuni zetu za Maadili ya Wauzaji

**Pata Maelezo Zaidi**

KBR Supplier Code of Conduct

Procurement and Supply Chain Management

# Tunaweka Rekodi na Akaunti Sahihi

Kuweka rekodi na akaunti sahihi kwa uadilifu kunaturuhusu kupangia siku za usoni na kuwapa hakikisho wadau wetu. Maamuzi na uwekezaji wa kimkakati hutegemea rekodi na akaunti zilizowekwa vizuri, na pia kutii sheria. Kama kampuni ya umma, tuna wajibu wa kutoa rekodi sahihi na kwa wakati unaofaa kwa wawekezaji na mashirika ya serikali kulingana na kanuni na sheria za nchi ambapo tunafanya kazi.

## Jinsi Tunavyoweka Rekodi na Akaunti Sahihi

- Kuweka mfumo wa vidhibiti vya ndani vya mahesabu vinavyotosha kutoa hakikisho linalofaa kuhusu uhakika wa ripoti za fedha
- Kutii kanuni za mahesabu zinazokubaliwa kwa jumla, masharti ya kisheria na vidhibiti vyote vya ndani
- Kudumisha akaunti, ripoti na risiti kwa njia ya kweli bila kuzibadilisha
- Kuhakikisha kwamba rekodi zote za mahesabu, ikijumuisha malipo yote, zinaonyesha kwa usahihi na haki miamala na uuzaji wa mali za kampuni
- Kuhakikisha kwamba miamala na uuzaji wote umeidhinishwa kwa mujibu wa sera na taratibu zetu na unaungwa mkono na hati za kuthibitisha uhalali wa miamala hiyo
- Kurekodi mali, madeni, mapato na gharama zote kikamilifu na kwa wakati unaofaa, hasa zinazohusiana na taarifa za fedha, ripoti na data iliyotayarishwa kwa ajili ya/au kama sehemu ya mchakato wa kuripoti wa ndani ya kampuni, wa umma na wa kisheria
- Kutoweka fedha au mali ambazo ni za siri au hazijarekodiwa
- Kuripoti masuala yoyote kuhusu rekodi zisizo sahihi au za kupotosha kwenye idara ya Ukaguzi wa Ndani (Internal Audit), Afisa Mkuu wa Mahesabu (Chief Accounting Officer), Idara ya Sheria, Timu ya Maadili ya Biashara, au Huduma ya Dharura ya Maadili
- Kufuata kanuni na sheria zote husika, ikijumuisha Sheria ya Sarbanes-Oxley, Sheria ya Desturi za Ufisadi za Kigeni (Foreign Corrupt Practices Act) na kanuni zozote zinazotumika za kupinga ufisadi au ulanguzi wa pesa



Mbali na rekodi za fedha, rekodi za kampuni zinaweza kuwa katika aina nyingi. Aina hizi zinajumuisha zifuatazo:

- Barua pepe, barua, memoranda, machapisho ya mitandao jamii, ujumbe wa maandishi na aina nyingine za mawasiliano
- Sera na taratibu
- Mikataba
- Ripoti, takwimu, fomula, ratiba na mawasiliasho
- Faili za binafsi

Tunapodhibiti rekodi zetu, tunafuata ratiba yetu ya muda wa kuhifadhi rekodi. Rekodi huhifadhiwa kwa vipindi maalum ili kuhakikisha zinapatikana ikiwa zinahitajika. Pia, tunatii masharti yote ya kisheria kuhusu rekodi za kampuni panapohitajika.

**Pata Maelezo Zaidi**

Content and Records Management Policy



# Kuthamini Jamii Zetu

- Tunajenga Mustakabali wa Kudumu
- Tunaheshimu Haki za Binadamu
- Tunashirikiana na Jamii Zetu



# Tunajenga Mustakabali wa Kudumu

Katika KBR, uendelevu ni muhimu katika shughuli zetu zote. Unaongoza mbinu yetu ya kusaidia jamii zetu, watu wetu na dunia yetu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Tunaendelea kujitahidi kubuni teknolojia mpya ambazo zinanufaisha dunia yetu. Suluhu zetu za kudumu zisizo na athari kwa mazingira, kama vile tekonolojia yetu ya urejeleshaji wa plastiki, zinasaidia kuunda mfumo wa uchumi wa mzunguko na kuturuhusu kuwasaidia wateja wetu kufanikisha malengo yao ya uendelevu. Kila mradi na shughuli ya biashara ni fursa ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya anga na kulinda na kurejesha ubora wa mazingira.

## Jinsi Tunavyojenga Mustakabali wa Kudumu

- Kujitolea kutumia mbinu za kisayansi za kupunguza utoaji wa gesi joto (GHG, Greenhouse Gas)
- Kushiriki katika Mradi wa Kimataifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Hali ya Anga wa Umoja wa Mataifa (United Nations Global Compact)
- Kupunguza athari mbaya kwa mazingira tunapoendeleza juhudi za kurejesha ubora wa mazingira
- Kujumuisha sera za mazingira na jamii katika kiini cha utamaduni wa KBR

**Pata Maelezo Zaidi**

Global Sustainability Policy

Global Environmental Policy

KBR Sustainability Pillar Commitments

KBR Zero Harm

KBR Sustainability



# Tunaheshimu Haki za Binadamu

Kama kampuni ya kimataifa, KBR inaheshimu na kudumisha viwango vya juu zaidi vya haki za binadamu na haikubali namna yoyote ya ukiukaji wa haki za binadamu. Tunatambua kwamba ulanguzi wa watu, utumwa wa kisasa na ajira ya watoto ni makosa mabaya sana. Tukiwa na maelfu ya wauzaji katika mamia ya nchi, tunachukua hatua za kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinaheshimiwa popote tunapofanya biashara. Kuthamini watu kunamaanisha kulinda hadhi ya binadamu katika jamii zetu zote.

## Jinsi Tunavyoheshimu Haki za Binadamu

- Kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wa KBR wanapewa saa za haki na zinazofaa na malipo kwa kazi yao katika mazingira salama
- Kufanya uchunguzi wa msingi ili kuhakikisha wauzaji na washirika wengine wanatii viwango vya ajira ya haki na haki za binadamu
- Kutokubali ajira ya watoto au utumikaji wa lazima popote duniani
- Kutumia tu kampuni au mashirika ya kuajiri wafanyakazi yanayotambulika
- Kuripoti haraka iwezekanavyo matukio ya ukiukaji wa haki za binadamu kwa Huduma ya Dharura ya Maadili, Timu ya Maadili ya Biashara au Idara ya Sheria
- Kufuata sheria, sera na taratibu zote zinazotumika, na kufanya kila tuwezalo ili kulinda hadhi ya binadamu

**Pata Maelezo Zaidi**

Global Human Rights Policy

Trafficking in Persons Policy

# Tunashirikiana na Jamii Zetu

Katika KBR, tunaamini kwamba ni wajibu wetu kuwa chanzo kizuri cha kuleta mabadiliko duniani. Tuna wajibu wa kuleta thamani ya jamii na kuchangia katika ustawi wa jamii za mahali tunapoishi na kufanya kazi. Katika kufanikisha dhamira yetu, tunalenga kila wakati kuunda ulimwengu bora na salama zaidi kwa ajili ya kila mtu.

## Jinsi Tunavyoshirikiana na Jamii Zetu

- Kujitolea na kushiriki katika shughuli za uhisani
- Kujitahidi kuleta athari nzuri ya kudumu katika jamii za eneo ambapo tunafanya kazi kupitia ushirikiano, mashauriano na mawasiliano
- Kufuata Taratibu zetu za Kupinga Ufisadi tunapotoa ufadhili wa kifedha au kufanya michango kwa jina la KBR
- Kudhibiti shughuli za kushirikisha jamii ili zilingane na maadili na wajibu wetu wa kazi

## Kusaidia Jamii

Tangu mwaka wa 2007, KBR imechangia takribani kiasi cha Dola Milioni 20 za Marekani ($20 million) ili kusaidia miradi ya uhisani duniani kote. Wafanyakazi wetu wamechanga nguo na vifaa vya shule ili kuwasaidia watoto maskini, kuchanga maelfu ya dola kwa ajili ya kununua zawadi za Krismasi kwa wasiojiweza, na kusaidia kusafisha mikondo ya maji na fuo duniani kote. Hii ni mifano kadhaa tu ya njia nyingi ambazo wafanyakazi wetu wamekuwa kiini cha kila kitu tunachofanya.

## Kushiriki katika Siasa

Sote tuna haki ya kushiriki katika mchakato wa kisiasa. Mfumo wazi wa kisiasa unachangia kubuni jamii yenye haki. Tunaposhiriki katika siasa:

- Tunatii kila wakati sheria zinazotumika kuhusu ushawishi wa kisiasa na michango ya kampeni
- Tunabainisha wazi kila wakati kwamba maoni yetu si maoni ya KBR
- Haturuhusu kamwe shughuli zetu za kisiasa kuathiri wajibu wetu kazini
- Hatulazimishi kamwe wafanyakazi wenzetu kujiunga na misimamo yetu ya kisiasa
- Hatutoi kamwe michango ya kisiasa kwa niaba ya KBR bila kuomba idhini mapema



# Nyenzo na Kuripoti

# Nyenzo na Kuripoti

Kama KBR MOJA, tumeunganishwa na lengo letu moja: kutekeleza kwa usalama mradi wowote, wakati wowote, katika mazingira yoyote kwa manufaa ya wateja wetu, wadau, wafanyakazi na jamii tunazohudumia. Kanuni zetu zinatupatia mwongozo tunaohitaji ili kujitahidi kufanikiwa kwa uadilifu. Kwa maelezo zaidi au ushauri, rejelea nyenzo zilizo hapa chini.

## Nyenzo za Jumla

BUSINESS INTEGRITY TEAM

- Timu ya Maadili ya Biashara
- Idara ya Sheria
- Huduma za Ukaguzi
- Kitengo cha Usimamizi wa Wafanyakazi (Rasilimali Watu)
- Afya, Usalama, Ulinzi na Mazingira
- Udumishaji wa Shirika

## Nyenzo za Kuripoti

- Huduma ya Dharura ya Maadili
    - Wavuti:
        - www.ethics.kbr.com
    - Piga simu:
        - Marekani: (800) 461-9330
        - Uingereza: 0808 189 1053
        - Kwa nambari za simu katika nchi nyingine zote, tembelea www.ethics.kbr.com
    - Tuma neno "Ripoti" kwa nambari 832-479-1340 (Inapatikana Marekani pekee)
- Barua pepe
    - FHOUKBR – CODE
    - fhoukbrcode@kbr.com
- Barua
    - Mkurugenzi wa Uadilifu wa Biashara, KBR, Inc.
    - P.O. Box 2464, Houston, TX 77252-2464 USA





Kutoa Suluhu, Kubadilisha Ulimwengu.℠